




**MKOA WA KIGOMA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU**  
**(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

Simu Na. +255 028 2810339  
 Fax Na. +255 028 2810339  
 E-Mail/Baruapep:ded@kasuludc.go.tz  
 Website:www.kasuludc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
 S. L. P 97,  
 Kasulu — Kigoma,  
**TANZANIA.**



Kumb Na. KSDC/S.2/21.Vol II/243

26/01/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu anapenda kuwatangazia watanzania wote kuwa Ofisi imepokea kibali cha Ajira Mbadala kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi chenye Kumb.Na.FA.170/358/01/C/57 cha tarehe 10 Agosti, 2021 kwa ajili ya kutangaza nafasi ya Mtendaji wa Kijiji III kwa masharti ya kudumu hivyo wenyе sifa mnaombwa kuomba nafasi ya kazi kama ifuatavyo:-

**1.0: MTENDAJI WA KIJJI DARAJA III (VEO III) - NAFASI 1**

**A: MAJUKUMU/KAZI ZA KUFANYA.**

- i) Afisa masuuli na Mtendaji wa serikali ya kijiji,
- ii) Kusimamia ulinzi wa Raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na usimamizi wa utawala bora,
- iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Jamii,
- iv) Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya kijiji,
- v) Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu,
- vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali,
- vii) Kiongozi wa wakuu wa vitengo katika kijiji, Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote za kijiji,
- viii) Mwenyekiti wa vikao vya wataalamu waliopo katika vijiji
- ix) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi,
- x) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**B: SIFA ZA KUAJIRIWA:**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV/VI aliyehudhuria na kuhitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (Certificate) katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, sheria, elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha serikali za mitaa Hombolo, Dodoma na chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

**C: NGAZI YA MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia viwango vya serikali ngazi ya mshahara ni TGS B kwa mwezi.

**D: MASHARTI YA JUMLA.**

- i) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania wenyе umri usiozidi miaka 45,
- ii) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye namba ya utambulisho wa uraia (NIDA)
- iii) Mwombaji anatakiwa kuambatisha nakala za vyeti vya Elimu ( Kidato cha IV/IV), vyeti vya Taaluma (Certificate), Cheti cha kuzaliwa na Wasifu (CV).
- iv) Transcripts "Testimonial, Provisional Results na statement of results havitakubaliwa.
- v) Barua za maombi ziandikwe kwa mkono na mwombaji mwenyewe na zitumwe kwa njia ya Posta tu, Mwisho wa kutuma na kupokelewa kwa maombi ni tarehe 11 Februari, 2022 saa 9:30 alasili kuititia anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
 HALMASHAURI YA WILAYA,  
 S.L.P 97,  
KASULU.**

Emmanuel Ladislaus

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
 HALMASHAURI YA WILAYA**

**KASULU DISTRICT COUNCIL  
 MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
 HALMASHAURI YA WILAYA  
 S. L. P. 97, KASULU**